
# PHUSIS

## KUYAENDEA MAISHA KUTOKEA KWENYE ASILI YA UUNGU YA MWAMINI



Pastor James Kalekwa

# PHUSIS:

*Kuyaendea Maisha Kutokea Asili ya Uungu ya Mwamini.*

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

**Tabaruku**.................................................................. 4

**Salamu na Utangulizi**.................................................... 5

**SURA YA KWANZA:**............................................................ 7

**UELEWA WA WALI KUHUSU ASILI YA UUNGU.** ..................... 7

**SURA YA PILI:**................................................................. 20

**KUJITAMBUA NA KUWATAMBUA WATU KWA JINSI YA ROHONI** ........................................................................ 20

**SURA YA TATU:**............................................................... 34

**KUWA KATIKA ROHO** ........................................................ 34

**SURA YA NNE:** ................................................................ 49

**NAMNA YA KUWA KATIKA ROHO**....................................... 49

**Kuhusu Mwandishi:** ......................................................... 56

**Kuhusu New Vine Church:** .............................................. 56

**Mawasiliano na Mwandishi:** ........................................... 57

# Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

# Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake **Juni 20**, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anavyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani huduma

yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2024
Dodoma, Tanzania

# SURA YA KWANZA:

# UELEWA WA WALI KUHUSU ASILI YA UUNGU.

*"Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa* ***washirika wa tabia ya Uungu****, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa."* 2 Pet 1:4 SUV

*"Kwa sababu hiyo, ametukirimia ahadi zake kuu na za thamani kupitia mambo haya, ili kupitia hayo mpate kuwa* ***washiriki wa asili ya uungu****, na kuokoka kutoka upotovu ulioko duniani unaosababishwa na tamaa mbaya."* 2 Petro 1:4 NEN

*"Kwa namna hiyo ametujalia zawadi kuu na za thamani ambazo alituahidia, ili kwa zawadi hizo mpate kuziepa kabisa tamaa mbaya zilizomo duniani, na kuishiriki* ***hali yake ya kimungu.****"* 2 Petro 1:4 BHN

Kwenye sura hii nimekusudia kwa msaada wa neno la Mungu (Maandiko Mtakatifu) na Roho Mtakatifu

tutazame hii asili ya uungu imetokea wapi na imetokana na nini. Tutakokotoa na kufikia kwenye hitimisho ambalo hautajitahidi sana kulikubali au kuliamini. Utafika mahali pa kujua kwa yakini kama uvavyojua jina lako au jinsi yako. Huna mashaka! Nisingependa uwe na mashaka na utambuzi wako wa asili ya uungu.

Hili neno tabia (SUV), asili (NEN) au hali (BHN) kwenye lugha ya Kiyunani husomeka '**Phusis**' (tamka *fuu-sis*) ambalo hubeba maana kadhaa.

- Asili ya kuzaliwa au kimaumbile (kuundwa/kutengenezwa/kuumbwa) – hii inamaanisha ni asili isiyogeuzwa, isiyoweza kubadilishwa. Imebeba maana na utambulisho.
- Jumla ya sifa za ndani na viwekezo ambavyo humtofautisha mtu mmoja na mtu mwingine (Vinasaba) – Hii inamaanisha vinavyounda mtu/kitu. Vinavozalisha upekee na umaalum wa mtu/kitu.
- Asili ya vitu; sheria ya asili; utaratibu wa asilia.
- Tofauti na kile kilichotengenezwa kwa mikono ya mwanadamu na/au kufanyiwa maboresho – Hii

inamaanisha kile kisichoweza kuhaririwa au kurekebishwa. Kiko pale na kinapaswa kupokelewa hivyo.

Kwa uelewa huo wa lugha asilia, ni sawa na kusema hii tabia/asili/hali ya uungu tuliyokirimiwa nayo ni sawa na kusema: N*diyo iko hivyo, hauna cha kufanya. Ni ama unaipokea au huopokei*.

*"Kanuni (asili) huwa hazivunjwi bali hupewa ushirikiano; Ukizivunja kanuni, utagundua unavunjika wewe na kanuni zinaendelea."* Bishop Goodluck Kyara

Kwa hiyo, kuhusiana na asili hakuna mjadala. Ni ama unakubaliana na kuanza kuishi kutokea hapo. Au unapingana (unajadiliana) na asili kwa hasara yako mwenyewe.

Mjadala wa asili umekwishakufungwa tayari. Kinachotakiwa kufanyika ni kuanza kuishi kuielekea. Hivyo ndivyo mwamini alivyo. Kama haishi kutokea kwenye asili hiyo ni kiashiria cha kukosa ufahamu tu. Ambacho hata hivyo hakiondoi hata chembe moja ya ukweli huu.

**Asili ya Uungu imetokeaje?**

a) Uumbaji – kwa mfano wa Mungu

*"Mungu akasema, Na tumfanye mtu* ***kwa mfano*** *wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba."* Mwa 1:26-27 SUV


**Tselem** – mfano wa; sanamu inayoelezea au kuwakilisha.

Hivi unajua asili ya Mungu ilikuwa ndani ya watu wa mwanzo kiasi kwamba ilikusudiwa wazae (kimwili na kiroho). Adamu na Hawa wangezaa watoto wenye asili ya utakatifu (bila kuwa na dhambi)?

Kiitifaki, kabla ya anguko ilikuwa hivi:

Mungu >>>> Mwanadamu >>>> Malaika (viumbe vya kiroho) >>>> Ulimwengu>>> Shetani

Ili kuwezesha uelewa kwa urahisi nimeambataisha taswira hapa kueleza dhana hii.




b) Anguko – Mtakuwa kama Mungu

*"lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke,* ***Hakika hamtakufa****, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo,* ***mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu****, mkijua mema na mabaya."* Mwa 3:3-5 SUV

Kuna kujua kama mtu wa chini (subordinate) kunakuja kwa kujulishwa na mtu wa juu yako/mwenye mamlaka halali juu yako.

Halafu kuna kujua kama mtu mwenye mamlaka ya juu ya watu wengine. Kutokana na kupambanua ili uwajulishe wengine kutokea kwenye nafasi ya mamlaka yako. Ujuzi huu hugeuka sheria na utaratibu wa maisha.

Mfano: Baba wa familia kwa kuwa ana taswira pana; Huweka utaratibu wa kuamka, kulala, kula, uelekeo wa malango ya fahamu ya familia, makatazo, nidhamu n.k... Lengo siyo kuwabania watoto wake kwa kuwa hawapendi (japokuwa wengine watamuona kama mkoloni). Lengo ni wawe watu bora. Kwa faida yao wenyewe.

Ujuzi wake hugeuka sheria... mema na mabaya.

Sasa, Adamu na Hawa walikuwa kwenye ngazi ya watoto wa familia... wanajua mema na mabaya (kwa kujulishwa na mwenye mamlaka juu yao).

Mtoto anapojiamulia muda wa kurudi nyumbani, namna ya kuvaa, nini atazame, lugha ya kuzungumza... anatuma ujumbe ya kwamba anataka kujiamulia mwenyewe kuhusu mema na mabaya yake (He’s redifining his own world/setting new boundaries). Ni ujumbe ya kwamba anataka kuwa baba... anajua mema na mabaya (siyo kwa

kuambiwa bali kwa kujiamulia). Hakuna nyumba yenye baba wawili ufahamu.

Hilo tendo linaitwa uasi.


*“Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi.”* 1 Yoh 3:4 SUV

Kile walichokifanya Adamu na Hawa ni UASI. Siyo walitaka kuwa kama Mungu. Bali walitaka kuwa Mungu wakijiamulia mema na mabaya. Umeelewa dhana hiyo ya kujua (kuamua) mema na mabaya?

Itifaki baada ya ANGUKO:

Mungu >>>> Malaika/Viumbe vya kiroho >>>> Shetani >>>> Uumbaji >>>> Mwanadamu

Ili kurahisisha uelewa wa namna gani itifaki iligeuzwa baada ya anguko,nimekuambatanishia taswira hapo chini.




MUHIMU: Mtu ambaye hajaokoka siyo tu anafanya dhambi (kama tendo) bali ana asili ya dhambi... mwenye asili ya dhambi hawezi kabisa kufanya tendo/tukio lenye haki. Hata matendo yake mema huwa ni dhambi kwa sababu ya asili aliyotenda kwayo. Hakuna matendo ambayo yanamwezesha mtu mwenye asili ya dhambi kuhesabika ya kuwa ni mwenye haki. Hapa swala ni asili siyo tendo tu!

c) Wokovu – Uwezo wa kufanyika wana wa Mungu

*“Bali wote waliompokea **aliwapa uwezo** wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake;”* Yn 1:12 SUV

Ni muhimu itambulike kwako mapema huu uwezo ni wa kupewa. Siyo uwezo unaotokana na mwanadamu mwenyewe (Sponsored faith).

Uwezo: exousia

- Nguvu au uwezo wa uchaguzi; kutenda kama mtu aonavyo vyema.
- Nafasi, hadhi, upendeleo au kufadhiliwa (Priviledge)
- Uwezo utokao ndani (capacity)
- Uwezo wa kutenda na kuleta matokeo (Competence)

*“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! **Yamekuwa mapya.**”* 2 Kor 5:17 SUV

Fikiria zaidi kwa upana kuhusu haya:

*"aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo"* Efe 1:20-22 SUV

*"Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu;"* Efe 2:6 SUV

Maandiko hayo awali yanaonyesha mchakato uliotumika ili kumpatia mwanadamu uwezo na kumbadilishia asili. Kutoka kwenye asili ya dhambi iliyotokana na anguko la kitabu cha Mwanzo 3.

Ni vyema utambue ya kwamba nusu ya kwanza ya kitabu cha Waefeso (Sura ya 1-3) kinashughulika na ASILI/UTAMBULISHO wa mwamini (Conceptual Theology);

Kisha nusu ya pili ya kitabu hicho (Sura 4-6) inashughulika na namna ya kuyaendea maisha kutokea kwenye asili hii (Practial Theology)


Kwa hiyo, wokovu ni badiliko la asili... wewe ni kiumbe kipya. Siyo tendo... ni asili!

Wewe mwenye asili ya uungu umeketishwa pamoja na Yesu katika ulimwengu wa roho.

Itifaki baada ya wokovu:

Mungu >>> Mwanadamu >>> Malaika >>> Shetani >>>> Ulimwengu

Ili kuwezesha kuelewa kwa urahisi mtiririko huu mpya wa kiitifaki kwa mtu aliyegeuzwa asili; mtu aliyeokoka tu. Nimeambatanisha taswira hapa chini.




Kama hiyo ndiyo asili yangu. Huo ndiyo mtiririko wa kiitifaki. Kama hivyo ndivyo nilivyo... tatizo ni nini? Umewahi kuwasikia vijana wakitumia huu msemo, *"Unakwama wapi?"* wakimaanisha ya kwamba kila kitu kinatenda kazi upande wako kukuwezesha lakini ni kama vile matokeo hayajafika mahali ambapo yanapaswa kuwa.

Sasa ndivyo ilivyo hapa… kama hii ndiyo asili yangu, tatizo ni nini?

*"Hawajui wala hawafahamu, hutembea gizani; Misingi yote ya nchi imetikisika. Mimi nimesema, Ndinyi miungu, Na wana wa Aliye juu, nyote pia. Lakini mtakufa kama wanadamu, Mtaanguka kama mmoja wa wakuu."* Zab 82:5-7 SUV

Tatizo: Hawajui wala hawafahamu

Matokeo: Kufa kama wanadamu, kuanguka kama mmoja wa wakuu.

Tatizo la kutokujua linapelekea matatizo mengine mengi kama vile ni namna gani huyaendea maisha.

# SURA YA PILI:

# KUJITAMBUA NA KUWATAMBUA WATU KWA JINSI YA ROHONI

*"Hata imekuwa, sisi tangu sasa* ***hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili.*** *Ingawa sisi tumemtambua Kristo kwa jinsi ya mwili, lakini sasa hatumtambui hivi tena."*

2 Kor 5:16 SUV

Kwenye sura hii nimekusudia tusogee hatua moja mbele baada ya kukokotoa asili ya uungu ndani yako kama mwamini. Hapa tutaanza namna gani ya kuenenda kutokea kwenye utambuzi huo.

Kutokea kwenye andiko la utangulizi la sura hii, watu ni zaidi ya miili na mwonekano wa nje. Kimsingi, watu halisi ni roho. Hebu tazama maandiko haya:

*"BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi,* ***akampulizia puani pumzi ya uhai****; mtu akawa nafsi hai."*
Mwa 2:7 SUV

na miili ni nyumba tu za watu kukaa roho iwapo duniani.

*"Kwa maana twajua ya kuwa* ***nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii*** *ikiharibiwa, tunalo jengo litokalo kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele mbinguni. Maana* ***katika nyumba hii*** *twaugua, tukitamani sana* ***kuvikwa kao letu*** *litokalo mbinguni; ikiwa tukiisha kuvikwa hatutaonekana tu uchi. Kwa sababu sisi tulio katika* ***maskani hii*** *twaugua, tukilemewa; si kwamba twataka kuvuliwa, bali kuvikwa, ili kitu kile kipatikanacho na mauti kimezwe na uzima."* 2 Kor 5:1-4 SUV

Mtume Paulo anafanya ulinganifu wa maskani mbili; makao mawili; nyumba mbili – mwili upatikanao na mauti (mortal body) na mwili usiopatikana na mauti (immortal body). Kutokea hapo utagundua mtu halisi na mwili ni wawili tofauti. Kwa mwanga wa andiko hilo utaelewa ya kwamba roho (mtu halisi) itabadilisha nyumba ya kukaa (mwili).

Kwa hiyo, mwanadamu ni zaidi ya mwili. Mwanadamu ni roho… Wewe ni roho!

Niakuambatanishia mifano kadhaa hapa ili kujenga uelewa juu ya dhana hii ya mwanadamu halisi ni roho na mwili ni nyumba yake.

Mfano #1: Tumepewa mtoto mwanamume (a son is given)

*"Maana kwa ajili yetu* ***mtoto amezaliwa****,* ***Tumepewa mtoto mwanamume****; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani."* Isa 9:6 SUV

*"For to us* ***a child is born****, to us* ***a son is given****, and the government will be on his shoulders. And he will be called Wonderful Counselor, Mighty God, Everlasting Father, Prince of Peace."* Isaiah 9:6 NIV

Hebu fikiria unafika mahali unasikia wasifu unasomwa kumuhusu mtu fulani: mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa Amani. Ni wasifu mzuri kweli. Unasubiri umuone mtu mwnye wasifu huo… itakushangaza sana kupokea taarifa kwamba mwenye wasifu hajazaliwa bado! Ulitaka uone mwili/umbo na

kumbe umesomewa wasifu wa roho. A child is born (mwili); A son is given (roho)!

Mfano #2: Mtu kutoka kwa Bwana

*"Palitokea **mtu**, ametumwa **kutoka kwa Mungu**, **jina lake Yohana.**"* Yn 1:6 SUV

Umesoma vyema… mtu kutoka kwa Mungu. Halafu unaona tena ana jina la kibinadamu kabisa. Kuna utambulisho wake wa kiroho (mtu kutoka kwa Mungu) halafu kuna utambulisho wake wa kimwili (Jina lake Yohana). Ukisoma kwenye Injili ya Luka 1:5-18; 23-25 utaona ni kwa namna gani mtu huyo alizaliwa… kama wanadamu wengine tu.

Sasa ni muhimu ukajua hili: kilichozaliwa hapo ni mwili siyo roho. Na watu wa rohoni tumejifunza kuangalia zaidi ya nyumba, kao, maskani iitwayo mwili – unanielewa?

Tusogee kwenye mfano unaofuatia hapa ili kuchora mstari unaotenganisha baina ya roho (ambaye ndiye mtu halisi) na mwili (ambalo ni kao la roho ya mtu awapo hapa duniani).

Mfano #3: Nabii wa Mataifa

*“Ndipo niliposema, Aa, Bwana MUNGU! Tazama, siwezi kusema;* ***maana mimi ni mtoto****. Lakini BWANA akaniambia,* ***Usiseme, Mimi ni mtoto****; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru.”* Yer 1:6-7 SUV

Je , ni kweli Yeremia alikuwa ni mtoto (mdogo kiumri kulinganisha na jukumu alilokuwa anapewa)?

Je, Mungu alisema kweli kwamba Yeremia si mtoto (tena Mungu alisema kwa lugha ya kukema)?

Iko hivi, Yeremia alikuwa anaongea kutokea kwenye utambulisho wa kimwili – umri na umbo la mwili wake, kwa taratibu za hapa duniani, alikuwa ni mtoto. Hata hivyo jinsi Mungu alivyokuja juu sana na kukemea huo usemi wa Yeremia, “Usiseme, Mimi ni mtoto!” ni kama anamwambia, "Funga kinywa. Ninajua ninachokifanya!”. Mungu anaongelea utambulisho wa roho ambaye ndiye Yeremia halisi.

Yeremia wa utambulisho wa roho ni nabii wa mataifa na kuna majukumu ya kung’oa, kuharibu ili kupanda… ana

majukumu mazito sana. Halafu Yeremia wa mwili ni mtoto mdogo – wazazi wake, ndugu na jamii yake ndiyo humtazama hivyo.

Mfano #4: Shujaa na mwokozi

*“Malaika wa BWANA akamtokea, akamwambia, BWANA yu pamoja nawe, **Ee shujaa.** BWANA akamtazama, akasema, **Enenda kwa uwezo wako huu, ukawaokoe** Israeli na mkono wa Midiani. Je! Si mimi ninayekutuma?”* Amu 6:12, 14 SUV

Kwenye utambulisho wa roho, Gideoni anatambulika kama shujaa na anao uwezesho wa kuwaokoa Israeli kutoka kwa Wamidiani. Lakini hebu tazama mwitikio wake:

*“Akamwambia, Ee Bwaba, nitawaokoa Israeli kwa jinsi gani? **Tazama, jamaa zangu ndio walio maskini sana katika Manase, na mimi ndimi niliye mdogo katika nyumba ya baba yangu**.”* Amu 6:15 SUV

Yeye anajitambua na kujitambulisha kwa hadhi na mwonekano wa mwilini – familia maskini na ya kwamba yeye ni mtoto wa mwisho!

Swali langu kubwa baada ya kukuwasilishia mifano hiyo, je huwa unajitambua na kujitambulishaje? Je, huwa unawapokea watu wengine kutokea kwenye uelewa wa namna gani? Roho au Mwili?

Ukitambua ya kwamba watu ni zaidi ya miili, mwonekano, maumbile, rangi, kabila, matamshi… watu halisi ni roho. Utajifunza kutazama zaidi (beyond) ya miili. Utakataa kutegwa na mwili wako na wa mtu awaye yote. Si ajabu mtume Paulo anasema, "…*sisi tangu sasa* ***hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili…***"

Tusogee mbele kidogo tena kwa kutazama mifano kadhaa ya watu waliojitambua kutokea kwenye nafasi zao za kiroho kiasi cha kuathiri namna gani walivyotenda kwa upande mmoja. Na wa upande wa pili tutaangalia ni namna gani watu waliwalewa wengine na kuwapokea kwa nafasi zao za kiroho kiasi cha kunufaika sana na hazina zilizobebwa na roho husika ndani ya makao/maskani/nyumba za hapa duniani yaani miili.

Halafu kutokea kwenye hiyo mifano utagundua moto utaanza kuwaka kwenye mifupa yako kwa jina la Yesu Kristo.

Mifano ya watu, nafasi na utendaji wao katika roho:

Mfano #1: Yusufu kama baba kwa Farao

*"Basi si ninyi mlionipeleka huku,* ***ila Mungu****; naye* ***ameniweka kama baba kwa Farao, na bwana katika nyumba yake yote, na mtawala katika nchi yote ya Misri****."* Mwa 45:8 SUV

Hebu subiri kwanza…! Hayo uliyoyasoma ni maneno mazito sana. Huyu ni Yusufu mwana wa Yakobo baada ya kukutana na nduguze anawapa *breaking news*. Anataka kwanza wajue ya kuwa yeye haoni kwamba ni wao ndiyo walimuuza bali ni Mungu ndiye alimleta huko. Sasa angalia sababu za Yusufu kuwa Misri:

a) Baba kwa Farao
b) Bwana kwa nyumba yote ya Farao
c) Mtawala wa ncho yote ya Misri

Umewahi kusoma Biblia mpaka ukapige yowe kwa sauti ya juu huku umeshika kichwa? Ndicho kilichonitokea siku nilipokutana na andiko hili. Yusufu anajielewa kiasi hicho. Yeye ni baba wa mfalme wa Misri- Farao. Kiumri, Yusufu ni mdogo kwa Farao; Kimamlaka, Yusufu ni mdogo kwa Farao; Kiuzoefu, Yusufu ni mdogo kwa Farao… lakini anatambua yeye ni baba!

Unakumbuka zile ndoto mbili alizoota (Mwanzo 37:5-9) akiwa pamoja nayo nyumbani kwa mzee Yakobo? Unakumbuka alipowasimulia ziliwasha masikio na kukereketa (Mwanzo 37:5,8)? – si tu kwa kaka zake ni mpaka baba yake (Mwanzo 37:10)! Unakumbuka kaka zake walimuita jina la *"bwana wa ndoto"* (Mwanzo 37:19)?

Kama hayo yaliwakera basi hapa anafungua kinywa chake tena kuwakera zaidi! Hakuwa anajitungia maneno na kutamka bila kuwaza vyema. Bali alikuwa anaongea kutokea kwenye uelewa wa yeye ni nani katika roho. Ufahamu huo ulipelekea ni kwa namna gani aenende.

Mfano # 2: Mlawi anayegombaniwa.

*"Mika akamwambia, kaa pamoja nami***, uwe kwangu baba, tena kuhani***, nami nitakupa fedha kumi mwaka kwa mwaka, na nguo ya kuvaa, na vyakula. Basi huyo Mlawi akaingia ndani. Ndipo Mika akasema,* ***Sasa najua ya kwamba BWANA atanitendea mema, kwa kuwa nina Mlawi kuwa kuhani wangu****."* Amu 17:10, 13 SUV

Kuielewa vizuri simulizi hii na mafunzo yake ni vyema ukachukua Biblia yako na kusoma sura ya 17 ya kitabu cha waamuzi chote. Huyu ndugu Mika alikuwa anaishi nje ya mji (Vilima vya Efraimu); ikatokea Mlawi anatafuta eneo jipya la kuishi ugenini… akiwa katika hali ya kutafuta, akakutana na Mika. Ndipo Mika akampokea na kumkaribisha.

Sasa, fuata mtiririko wa simulizi hii: Mika anampokea awe a). Baba kwake b). Kuhani wa nyumba… Angalia gharama ambazo Mika alikuwa tayari kulipia ili mahitaji hayo yatimilizwe. Usisahau tulipotokea, Mlawi alikuwa anatafuta makazi lakini Mika hakumpokea kama mtu tu anayetafuta makazi. Ninachotaka uone hapa ni utambuzi

wa kiroho wa Mika. Hakupokea mgeni bali alikuwa anapokea baba na kuhani. Unanielewa? Halafu angalia hitimisho la Mika: "…***Sasa najua ya kwamba BWANA atanitendea mema, kwa kuwa nina Mlawi kuwa kuhani wangu****.*"

Utambuzi wa ajabu sana huu!

Unafikiri habari iliishia hapo? Tusogee mbele nikuonyeshe tena jambo. Ili uweze kupata taswira kubwa chukua tena Biblia na usome sura ya 18 yote ya kitabu cha Waamuzi.

*"Wao wakamwambia, Nyamaza wewe, weka mkono wako kinywani mwako, uende pamoja nasi,* ***uwe kwetu baba, tena kuhani****; je! Ni vema kwako kuwa kuhani kwa ajili ya nyumba ya mtu mmoja, au kuwa kuhani kwa ajili ya kabila na jamaa katika Israeli?"* Amu 18:19 SUV

Huyu anayezungumziwa hapa ndiye Mlawi yuleyule aliyepokelewa na Mika kwenye vilima vya Efraimu. Hili ni jeshi la jumla ya watu mia sita wakiwa kwenye misheni ya kuchukua mji… walienda kuchukua na Mlawi kwa ajili

ya kabila lao la Dani. Sasa angalia sababu zilizowafanya wamteke Mlawi ni ili awe a). baba b) kuhani.

Usingedhania wanajeshi "wana akili" za kiroho namna hii! Wanaitambua na kuiheshimu mamlaka ya kiroho… walimtazama yule Mlawi si kwa mwonekano bali kwa vile alivyo katika roho. Huwa ninapenda sana nikisoma mstari wa 17 -19 kuna picha huja ya misheni maalum (special mission) ya kijeshi.

Mfano #3: Mtume Paulo

*"kama wenye huzuni,* ***bali siku zote tu wenye furaha****; kama maskini,* ***bali tukitajirisha wengi****; kama wasio na kitu,* ***bali tu wenye vitu vyote****."* 2 Kor 6:10 SUV

Kuna mtiririko mrefu wa ulinganifu ambao mtume Paulo anaufanya hapa. Analinganisha mwonekano wa mwili na hali ya roho. Anazungumzia kundi la watumishi wa Mungu ambalo linaweza *"kukudanganya"* kwa mwonekano wao – kama wenye huzuni… kama maskini… kama wasio na kitu. Ndivyo yeye na wengine walivyokuwa wakionekana. Hata hivyo anaenda mbele na kuwasaidia wasiishie kutoa mahitimisho kwa kutazama

hali ya miili. Anaonyesha uzito waliobeba watumishi katika roho:

a) Wenye furaha siku zote
b) Tukitajirisha wengi
c) Tu wenye vitu vyote

Huwa ninawaambia vijana wanaoingia kwenye wito wa utumishi. Hii ni kazi ya hadhi na ya heshima kuliko kazi zote kuwahi kutokea duniani. Unaona Mtume Paulo alivyokuwa anajitambua kwa roho si mwili?

Mfano #4: Uambukizo wa kiroho

*"Enenda pamoja na* ***wenye hekima****, nawe* ***utakuwa na hekima;*** *Bali rafiki wa wapumbavu ataumia."* Mit 13:20 SUV

Nilifundishwa mapema sana jambo hili kwamba maisha yangu ya kiimani na kumfuata Bwana Yesu yanaathiriwa pakubwa na watu ninaombatana nao. Kwa sababu watu ni zaidi ya miili na mwonekano wa nje tu. Watu ni vile walivyo katika hali zao za kiroho. Hupaswi kupuuzia hali ya kiroho ya mtu kwa sababu kimsingi huyo ndiye mtu halisi.

Sasa, mwenye hekima anatuonyesha ya kwamba kuna uambukizo hutokea kwa mtu kutoka kwa mtu mwingine kwa sababu ya vile alivyo katika hadhi ya kiroho.

Kwa uelewa huo utaendelea kujichukulia kama mwananchi wa kawaida? Utaendelea kujitambulisha kuwa wewe ni mtu tu? Je, utaendelea kuwachukulia watu na kuwapokea kwa vile wanavyoonekana kwa nje?

Hatuwatambui tena watu kwa jinsi ya mwili!

Hatujitambui tena kwa jinsi ya mwili!

# SURA YA TATU:

# KUWA KATIKA ROHO

Kwenye sura hii nimekusudia tupige hatua ya mbele tena zaidi kuhusiana na ulimwengu wa roho. Tumeshajua asili na namna gani ilitokea… tumeshagundua ya kwamba tunapaswa kujitambua na kuwatambua watu kwa jinsi ya roho. Namna nyingine ya kuyaendea maisha ya siku kwa siku kutokea kwenye asili ya uungu ya mwamini ni kuwa katika roho!

Ulimwengu wa roho ni halisi na unatenda kazi (is in operation). Ile ya kwamba hauonekani kwa macho, haumaanishi kwamba haupo. Ile ya kwamba haushikiki kwa mwili, haimaanishi haupo… ndiyo maana ukaitwa ulimwengu wa **roho**.

Ulimwengu wa roho kuna viumbe, maeneo, shughuli na matukio yanaendelea kama kawaida. Ili uweze kunufaika nao ni lazima ujifunze kuwa katika roho.

Hebu tazama maandiko haya kisha tujadili jambo hapa.

*“Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, **nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo**, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu. **Nalikuwa katika Roho**, siku ya Bwana; nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu,”* Ufu 1:9-10 SUV

Angalia eneo alilokuwa Yohana

a) Alikuwa kisiwa cha Patmo
b) Alikuwa katika Roho

Mtu mmoja yuko kwenye maeneo mawili kwa wakati mmoja; eneo moja tunaweza kulitafuta kwenye ramani ya dunia na kulipata; Unaweza kulitafuta kwenye googlemap na kulipata; tunaweza kwenda na kufika... eneo jingine halijulikani na wanajiografia. Patmo na katika Roho!

“...nikasikia sauti kama sauti ya baragumi ikinena...”

Hiyo ni sauti wapi? Katika Roho... Hiyo sauti si pale Patmo bali ni kwenye eneo lile jingine ambalo alikuwepo.

*"ikisema, Haya uyaonayo uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba:* ***Efeso, na Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na Sardi, na Filadelfia, na Laodikia.****"* Ufu 1:11 SUV

Uyaandie katika na kuyapeleka? Wapi?... katika mwili. Hayo maeneo anayoyataja yapo mpaka sasa (ni nchi ya Uturuki ya sasa au Asia ndogo kwa zama za ramani ya Agano Jipya). Ni maeneo ya kijiografia.

Hebu tazama hizi kweli kutokea kwenye uelewa huo wa kimaandiko ili kukazia maarifa hapa:

- Alikuwa sehemu mbili kwa wakati mmoja (Patmo na katika Roho)
- Kuna mambo yanaendelea katika Roho (Sauti ya Baragumu na maelekezo mengi)
- Kuna mambo yanaendelea katika mwili (Amefungwa/Anatumikia kifungo)
- Mambo katika Roho yanatakiwa yajulikane katika mwili na yaathiri kinachoendelea katika mwili.

Hebu tuangazie macho kiasi walau kwa njia ya dondoo kuhusiana na ulimwengu wa roho na mapana yake:

i. Ulimwengu wa roho ni halisi sana – kwa sababu umekuwepo kabla ya ulimwengu wa mwili na ndiyo umeuumba ulimwengu wa mwili (Kama unaamini ulimwengu wa mwili ni halisi basi ule wa roho ni halisi sana). Huwa ninatumia mfano huu kurahisisha kazi ya uelewa: Ile ya kwamba umeniona mimi Pastor JK basi unapaswa kuamini ya kwamba baba yangu ni halisi… Yupo tu! Hata kama humjui au hujawahi kuonana naye. Kimsingi, yeye ni halisi zaidi kuliko mimi. Hakuna mtoto aliyejizaa mwenyewe.

ii. Ulimwengu wa roho una nguvu kuliko ulimwengu wa mwili – huutawala ulimwengu wa mwili. Mambo katika ulimwengu wa mwili huendeshwa kw aufahamu wa uwepo wa ulimwengu wa roho na namna ya kuhusiana nao.

iii. Ulimwengu wa roho ulikuwepo kabla na utakuwepo hata baada ya ulimwengu wa mwili. Ulimwengu wa roho ni wa milele – hauna mwanzo wala hautakuwa na mwisho (ni wa milele). Wakati ulimwengu wa mwili ni wa kitambo – Una mwanzo na hatimaye utakuwa na mwisho wake.

Kwa hiyo, ulimwengu wa roho siyo dhania (mere imaginations). Bali ni halisi sana. Ni ulimwengu ambao uko hai na kuna mambo yanaendelea hata sasa. Hapa nitaambatanisha maandiko mengi ili kuthibitisha uwepo na uahlisia wa ulimwengu wa roho. Ni vyema ukasoma kila aandiko na kusikia sauti ya neno na roho nyuma ya andiko husika.

Hebu tazama:

*"Namjua mtu mmoja katika Kristo, yapata sasa miaka kumi na minne, (kwamba alikuwa katika mwili sijui; kwamba alikuwa nje ya mwili sijui; Mungu ajua). Mtu huyo alinyakuliwa juu mpaka mbingu ya tatu. Nami namjua mtu huyo, (kwamba alikuwa katika mwili sijui; kwamba alikuwa nje ya mwili sijui; Mungu ajua); ya kuwa alinyakuliwa mpaka Peponi, akasikia maneno yasiyotamkika, ambayo haijuzu mwanadamu ayanene. Kwa habari za mtu kama huyo nitajisifu; lakini kwa ajili ya nafsi yangu sitajisifu, isipokuwa katika habari ya udhaifu wangu."* 2 Kor 12:2-5 SUV

*"Ndipo roho ikaniinua, nami nikasikia nyuma yangu sauti kama mshindo wa radi kuu, ikisema, Na uhimidiwe utukufu wa BWANA tokea mahali pake."* Eze 3:12 SUV

*"Basi roho ikaniinua, ikanichukua mahali pengine; nami nikaenda kwa uchungu, na hasira kali rohoni mwangu, na mkono wa BWANA ulikuwa juu yangu kwa nguvu."* Eze 3:14 SUV

*"Na roho hiyo ikaniinua, ikanichukua katika maono, kwa nguvu za roho ya Mungu, hata Ukaldayo, kwa watu wale wa uhamisho. Basi maono niliyoyaona yakaniacha. Ndipo nikawaambia watu wa uhamisho habari ya mambo yote aliyonionyesha BWANA."* Eze 11:24-25 SUV

*"Kisha Roho ikaniinua, ikanichukua mpaka ua wa ndani; na tazama, utukufu wa BWANA uliijaza nyumba."* Eze 43:5 SUV

Baada ya kuutambua uhalisia wa ulimwengu wa roho, ni vyema pia nikuonyeshe ya kwamba kuna mambo kadhaa

ambayo huendelea katika ulimwengu wa roho ili usiwe mtu asiyejua juuya nini kianendelea.

i. Kuna shughuli zinaendelea. Ulimwengu wa roho umetingwa na shughuli nyingi (the spiritual realm is full of activities). Kuna missions; assignments; mitembeo; mibadilishano; ajenda na utekelezaji wake; maazimio n.k Hebu tazama mfano huu mzuri kwenye kitabu cha Danieli

*"Basi hapo nilipokuwa nikisema, na kuomba, na kuiungama dhambi yangu, na dhambi ya watu wangu Israeli, na kuomba dua yangu mbele za BWANA, Mungu wangu, kwa ajili ya mlima mtakatifu wa Mungu wangu; naam, nilipokuwa nikinena katika kuomba, mtu yule, Gabrieli, niliyemwona katika njozi hapo kwanza, akirushwa upesi, alinigusa panapo wakati wa dhabihu ya jioni. Akaniagiza, akaongea nami, akasema, Ee Danieli, nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu. Mwanzo wa maombi yako ilitolewa amri, nami nimekuja kukupasha habari; maana wewe unapendwa sana; basi itafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya."* Dan 9:20-23 SUV

ii. Kuna kalenda na mpangilio wa nyakati na majira (na matukio husika).

Kama ilivyo halisi kwamba katika mwili kuna kalenda na matukio. Ndivyo ilivyo halisi sana katika roho kwamba kuna kalenda na matukio... siyo matukio yote katika kalenda ya mwili huwa unashiriki; unazingatia; unafuatilia... lakini mengi yanakuathiri moja kwa moja. Hususani yaliyo kwenye mamlaka ya kiutawala unamoishi (jurisdiction)... Kwa hapa kwetu Tanzania kuna sikukuu kama vile: Siku ya Uhuru -9 Dessemba; Sikukuu ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar - Aprili 26; Nyerere Day; Karume Day; Nane Nane; Sabasaba na nyinginezo nyingi

Hata kama wewe unadhani hazikuhusu au hauzisherehekei, zitakuathiri kwa namna moja au nyingine. Haiwezekani kuwe na sikukuu nchini ambayo haitayaathiri maisha yako.

Ndivyo ilivyo, katika ulimwengu wa roho kuna mpangilio na uratibu makini wa matukio ya kikalenda.

*“Akaniagiza, akaongea nami, akasema, Ee Danieli, nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu. Mwanzo wa maombi yako ilitolewa amri, nami nimekuja kukupasha habari; maana wewe unapendwa sana; basi itafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya.* ***Muda wa majuma sabini*** *umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu, ili kukomesha makosa, na kuishiliza dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu, na kuleta haki ya milele, na kutia muhuri maono na unabii, na kumtia mafuta yeye aliye mtakatifu. Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu;* ***kutakuwa na majuma saba****; na katika* ***majuma sitini na mawili*** *utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu. Na baada ya yale* ***majuma sitini na mawili****, masihi atakatiliwa mbali, naye atakuwa hana kitu; na watu wa mkuu atakayekuja watauangamiza mji, na patakatifu; na mwisho wake utakuwa pamoja na gharika, na hata mwisho ule vita vitakuwapo; ukiwa umekwisha kukusudiwa. Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa* ***muda wa juma moja****; na* ***kwa nusu ya juma*** *hiyo*

*ataikomesha sadaka na dhabihu; na mahali pake litasimama chukizo la uharibifu; na hivyo, hata ukomo, na ghadhabu iliyokusudiwa imemwagwa juu yake mwenye kuharibu."* Dan 9:22-27 SUV

iii. Kuna uhalisia wa kimaisha (There are realities of life in the spiritual realm)

Case: Ufalme wa Israeli (Yuda)

*"Ndipo akaniambia, Usiogope, Danieli; kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, maneno yako yalisikiwa; nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako.* ***Lakini mkuu wa ufalme wa Uajemi alinipinga siku ishirini na moja;*** *bali, tazama,* ***huyo Mikaeli, mmoja wa hao wakuu wa mbele, akaja kunisaidia****; nami* ***nikamwacha huko pamoja na wafalme wa Uajemi****. Ndipo akasema, Je! Unajua sababu hata nikakujia? Na sasa nitarudi ili nipigane na mkuu wa Uajemi; nami nitakapotoka huku,* ***tazama, mkuu wa Uyunani atakuja.*** *Lakini nitakuambia yaliyoandikwa katika maandiko ya*

*kweli; wala hapana anisaidiaye juu ya hao ila huyo Mikaeli, mkuu wenu.”* Dan 10:12-13, 20-21 SUV

*“**nimwambiaye Koreshi, Mchungaji wangu, naye atayatenda mapenzi yangu;** hata ataunena Yerusalemu, Utajengwa; na hilo hekalu, Msingi wako utawekwa.”* Isa 44:28 SUV

*“Haya ndiyo BWANA amwambiayo Koreshi, masihi wake, ambaye nimemshika mkono wake wa kuume, ili kutiisha mataifa mbele yake, nami nitalegeza viuno vya wafalme; ili kufungua milango mbele yake, hata malango hayatafungwa. Kwa ajili ya Yakobo, mtumishi wangu, na Israeli, mteule wangu, nimekuita kwa jina lako; nimekupa jina la sifa; ijapokuwa hukunijua. Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine; zaidi yangu mimi hapana Mungu; nitakufunga mshipi ijapokuwa hukunijua;”* Isa 45:1, 4-5 SUV

*“Ikawa katika mwaka wa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi, ili kwamba neno la BWANA alilolisema kwa*

*kinywa cha Yeremia lipate kutimizwa, BWANA akamwamsha roho yake Koreshi, mfalme wa Uajemi, hata akapiga mbiu katika ufalme wake wote, akaiandika pia, akisema, Koreshi, mfalme wa Uajemi asema hivi; BWANA, Mungu wa mbinguni, amenipa falme zote za dunia; naye ameniagiza nimjengee nyumba katika Yerusalemu, ulioko Yuda. Basi kila mtu katika ninyi nyote mlio watu wake, BWANA, Mungu wake, na awe pamoja naye, na akwee mpaka Yerusalemu, ulioko Yuda, akaijenge nyumba ya BWANA, Mungu wa Israeli, (yeye ndiye Mungu), iliyoko Yerusalemu. Na mtu awaye yote aliyesalia mahali po pote akaapo hali ya ugeni, na asaidiwe na watu wa mahali pake, kwa fedha, na dhahabu, na mali, na wanyama, zaidi ya vitu vitolewavyo kwa hiari ya mtu, kwa ajili ya nyumba ya Mungu, iliyoko Yerusalemu."* Ezr 1:1-4 SUV

*"Tena Koreshi, mfalme, alivitoa vyombo vya nyumba ya BWANA, alivyokuwa amevileta Nebukadreza toka Yerusalemu, na kuvitia katika nyumba ya miungu yake. Naam, vyombo vile ndivyo alivyovitoa Koreshi, mfalme*

*wa Uajemi, kwa mkono wa Mithredathi, mtunza hazina; naye akavihesabu mbele ya Sheshbaza, mkuu wa Yuda."* Ezr 1:7-8 SUV

Kuna shughuli nyingi sana ziliendelea kwenye ulimwengu wa roho ili taifa la Israeli lijpatie uhuru kutoka kwenye uteka waliochukuliwa na Babeli na kuhamishwa. Danieli kama mwombaji alikuwa tayari kulipa gharama ya kuushughulisha ulimwengu wa roho mpaka matokeo yashikike katika ulimwengu wa mwili.

iv. Kuna uwezekano mwingi zaidi ya ule uliopo katika mwili (There are many possibilities).

*"Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe. Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire, kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa BWANA itapatikana."*Mwa 22:13-14 SUV

*“Naye akaogopa akasema, Mahali hapa panatisha kama nini! Bila shaka, hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndipo lango la mbinguni.”* Mwa 28:17 SUV

Kuna mambo ambayo kwenye ulimwengu wa mwili ni ukomo na hayawezekani kupatikana tena. Hata hivyo, ulimwengu wa roho unaweza kuzalisha mambo kiasi cha kushikika kwenye ulimwengu wa mwili. Hebu jiulize hivi, yule mwanakondoo wa sadaka alitokea wapi?

Tazama kile anachokisema Yakobo: Hapa ni nyumba ya Mungu; Hapa ndipo lango la mbinguni. Lakini hakujua na watu wengine walikuwa hawajui.

Ninataka uone possibilities hizo zilivyo katika ulimwengu wa roho. Kuna milango… kuna upaji wa Mungu. Ni vile tu ulimwengu wa mwili umezuiliwa (limited with possibilities).

Sasa mtu anayeenda kutokea kwenye asili ya uungu ana utambuzi huu kuhusu ulimwengu wa roho na kwa sababu hiyo hazuiliwi na yale yanayoonekana tu. Ili uenende katika asili ya uungu ambayo umeshirikishwa tayari na Bwana Yesu Kristo, ni vyema uwe katika roho.

Kuwa katika roho ni nini?

- Ni kuwa na utambuzi wa juu kuhusiana na uwepo wa ulimwengu wa roho na uhalisia wake. (High sensitivity).
- Kuwa hai (alive and active) kwa kujua na kukusudia katika maswala ya ulimwengu wa roho.
- Kuwa na shauku kuwa mshiriki na mnufaika wa yanayoendelea katika roho.

Kuwa katika roho si kuwa kituko au mazingaombwe kama ambavyo wengi wangedhani. Ninatambua ni kawaida ya akili ya mwanadamu kukataa mambo marahisi… hata hivyo, kuwa katika roho ndiyo rahisi namna hiyo.

# SURA YA NNE:

# NAMNA YA KUWA KATIKA ROHO

1. Kuwa na uelewa kuhusu uhalisia wa ulimwengu wa roho.

Hii ni kanuni muhimu sana ya kwamba huwezi kutenda zaidi ya kiwango cha maarifa kilichomo ndani yako kuhusiana na uwepo, uhalisia na utendaji wa ulimwengu wa roho. Kimsingi, maarifa ndani yako ndiyo hukuendesha kutenda jambo fulani. Kwa hiyo, unapaswa kujikusanyia mafundisho kama haya kuhusiana na uliwemngu wa roho. Hususani kwenye

- Uhalali wako kutenda humo. Kutambua ya kwamba ni halali kwako kutenda katika ulimwengu wa roho.
- Nafasi yako ya mshiriki hai (active participant). Kujua haki na stahiki zako katika ushiriki wa shughuli za ulimwengu wa roho.

*"Asiyemcha Mungu humpoteza jirani yake kwa kinywa chake;* ***Bali wenye haki watapona kwa maarifa****."* Mit 11:9 SUV

Umenona kifaa cha Mungu kuwaponya weye haki? Ni maarifa!

*"… kwa kuwa umeyakataa maarifa, mimi name nitakukataa wewe…"* Hosea 4:6

Ujumbe wa Mungu mwenyewe kwa kinywa cha nabii Hosea. Ukiyakataa maarifa, hakuna namna utasaidika.

2. Kuwa kwenye upweke (muda binafsi na Mungu) – kujiepua/kujitenga na umati.

Nilifundishwa jambo hili mapema sana ya kwamba huwezi kujipambanua kwenye umati iwapo utakaa kama wao. Ya kwamba namna moja wapo ya kutambua kwamba umeshikiliwa na kuzuiliwa mahali ni kujisikia ridhiko kukaa muda mrefu na umati.

Watu wote wanaotenda kwa uhai kwenye ulimwengu wa roho ni waliojifunza sanaa ya kujitenga… kujiepua… kutengana na watu kwa muda.

*“Ajitengaye na wenzake* ***hutafuta matakwa yake mwenyewe****; Hushindana na kila shauri jema.”* Mit 18:1 SUV

Ndiyo, kuna mkazo wa andiko hilo kuhusiana na watu wanaopingana na mashauri mema. Ningependa tujifunze kwa uchanya kwa “wakosefu” hao. Kutafuta matakwa yako mwenyewe (pursuing your desires) kutakugharimu kujitenga na wenzako. Ndiyo gharama ya uhai wa kiroho.

*“Lakini yeye* ***alikuwa akijiepua****, akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba.”* Lk 5:16 SUV

*“Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka* ***akaenda zake mahali pasipokuwa na watu****, akaomba huko.”* Mk 1:35 SUV

Nyakati za upweke ni muhimu sana katika kuwajengea watu msuli wa rohoni – ungefanya nini ungekuwa kisiwa cha Patmo? Ungefanya nini ungekuwa kwenye tumbo la samaki siku 3? Ungefanya nini ungeitwa mlimani siku

zisizojulikana (siku 40)? Ungefanya nini ungepelekwa nyikani kwa siku 40?

Miaka 3 ya upweke ya Mtume Paulo akiwa Arabuni.

*"Kwa maana, ndugu zangu, injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu. Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo. Wala sikupanda kwenda Yerusalemu kwa hao waliokuwa mitume kabla yangu; bali nalikwenda zangu Arabuni, kisha nikarudi tena Dameski."* Gal 1:11-12, 17 SUV

3. Kuomba kwa muda mrefu – Lengo ni kuiwasha roho yako (utu wako wa ndani). Maombi ni tendo la ushirika wa kina baina ya mwanadamu na Mungu. Kwa hiyo, muda unaowekezwa kwenye maombi hufanya ushiriki wa mwanadamu kwenye uimwengu wa roho kuwa hai. Kwa kusema kuhusu maombi ya muda mrefu ninamaanisha mambo mawili, kwa uwiano na uzito sawia.

- Muda mrefu mfululizo – Hapa ninamaanisha kushika ajenda moja au hata ajenda kadhaa na kukaa nayo maombini kwa muda mrefu.
- Tabia (tena na tena) – Yesu; Petro na Yohana; Danieli. Hapa ninamaanisha kuwa na maombi kama vile tabia. Kuomba kwa kurudia rudia. Kuwa na ratiba ya kimaombi.

*"Akatoka akaenda mpaka mlima wa Mizeituni kama* ***ilivyokuwa desturi yake****; wanafunzi wake nao wakafuatana naye."* Lk 22:39 SUV

Umesoma kitabu changu kiitwacho ujenzi wa tabia? Tafuta usome kitafafanua vizuri eneo hili.

- Katika roho

*"Bali ninyi, wapenzi, mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu,"* Yud 1:20 SUV

Kuna kitabu kingine kinaitwa **kuomba katika roho**. Hapa ninamaanisha kuomba kwa kuendeshwa na kuvuviwa na Roho wa Mungu ndani yako. Ataachilia kina (intensity) cha kimaombi, maneno, lugha, msamiati wa

kuomba; Ataachilia shauku/usongo wa namna gani uombe.

Maombi ya namna hii husababisha hali ya kupambanua (discernment), kujua na kuelewa kwa namna ya kiroho.

4. Kuwa mtu mwanana

*"Tena* ***haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi****; bali* ***kuwa mwanana*** *kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu;"* 2 Tim 2:24 SUV

Haimpasi – ni sharti! Siyo maoni, siyo ombi, siyo pendekezo… ni sentensi inayodai. Ni takwa ambalo mtumishi wa Mungu anapaswa kuishi kulitimiza. Mtu mwanana maana yake ni:

- Mtu wa amani – yuko upande wa amani wa maswala (issues) na watu. Hata kama jambo lina ubaya ndani yake, mtu wa namna hii hutafuta kuuona na kuukuza upande wa Amani.
- Mtulivu- mwanana humaanisha pia hali ya utulivu (composure). Huyatenda na kuyaitikia mambo kwa utulivu.

*"Basi huyo mtu, huyo Musa, alikuwa* ***mpole sana*** *zaidi ya wanadamu wote waliokuwa juu ya uso wa nchi."* Hes 12:3 SUV

*"Angalieni, mimi nawatuma kama kondoo kati ya mbwa-mwitu; basi iweni na busara kama nyoka,* ***na kuwa watu wapole kama hua."*** Mt 10:16 SUV

- Usiyeshikilia uchungu/kinyongo – shina la uchungu. – Unakumbuka Simeoni na Lawi Mwanzo 49?
- Unaweza kuahirisha ghadhabu/hasira

*"Busara ya mtu* ***huiahirisha hasira yake****; Nayo ni fahari yake* ***kusamehe makosa****."* Mit 19:11 SUV

Wakati ninajifunza kwenye eneo hili kwa kufuatilia watumishi wa Mungu kwenye Biblia na kwenye nyakati nje ya Biblia, niligundua ya kwamba wengi ni watu mwanana kiasi kwamba watu wasiojua siri hii huwachukulia kwa ukawaida.

Mpendwa, kama utaenenda katika asili ya uungu, huwezi kuepuka siri hii.

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**



**NEW VINE CHURCH** | **Dodoma**



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

## Ratiba za Ibada

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni

**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa

+255 754 917 764

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

pastorjameskalekwa

MchungajiJK

+255 754 917 764